**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Nane – Tarehe 17 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

60. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika kuhakikisha kwamba sekta binafsi nayo inashiriki katika ujenzi wa uchumi wa nchi, Serikali yetu imeanzisha sera ya PPP ili kuhamasisha sekta na watu binafsi kushirikiana na serikali katika kutekeleza kazi za maendeleo, sera hiyo ina zaidi ya miaka 10.

(a) Je, ni miradi mingapi hadi sasa ambayo imetekelezwa kwa njia ya PPP.

(b) Je, Serikali haioni kwamba muda umefika kwa Hoteli ya Bwawani kutafuta wawekezaji wa kushirikiana na Serikali ili hoteli hiyo na eneo lake kubwa na zuri kuendelezwa kwa mpango wa PPP.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

39. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Vitambulisho vyetu vya Mzanzibari vinasomeka "Mzanzibari Mkaazi" badala ya kuitwa "Kitambulisho cha Mzanzibari"

Je, kuna sababu zipi zinazozuia kitambulisho hicho kuitwa "Kitambulisho cha Mzanzibari".

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

3. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uvamizi wa maeneo ya wazi kote nchini unaotokana na ujenzi holela wa makaazi ya wananchi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyarejesha maeneo hayo ya wazi katika uasili wake.

(b) Ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa watendaji wasio waaminifu wa Taasisi zinazotoa vibali vya ujenzi wa nyumba za makaazi kwa maeneo hayo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

103. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya Mangapwani, Zingwezingwe, Mahonda ni mbovu kwa muda mrefu na ukizingatia ina ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu Mhe.Dkt Ali Mohamed Shein.

Je, ni lini itajengwa barabara hii ili kuwaondoshea matatizo wananchi wa eneo hilo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

128. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Vijana) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 inasisitiza suala la vijana kujiajiri wenyewe ili kuepusha utegemezi wa ajira kutoka Serikalini. Licha ya jitihada hizo zinazochukuliwa na Serikali, bado wimbi la vijana kuomba ajira za Serikali limekuwa kubwa sana.

(a) Je, Serikali inatumia mikakati gani kuwajuilisha vijana kwamba kuna fedha maalum kwa ajili ya

mikopo ya vijana ili wajiwezeshe wenyewe kimaisha.

(b) Serikali imekuwa ikitumia mbinu gani kufanya tathmini kwamba mikopo na fedha walizotoa kwa vijana zimekuwa zikitolewa kwa malengo yaliyokusudiwa kwenye kujiajiri wenyewe.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

118. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Lengo la Serikali ni kuwafanyia wepesi wa maisha wananchi wa kipato cha chini lakini wanaonekana kusumbuka na kutomudu gharama za ujenzi ikiwa ni pamoja na kutoimudu bei ya mchanga. Katika biashara hiyo ya mchanga mwananchi wanaokodisha ardhi kwa Serikali hupata faida ndogo ya ukodishwaji wa maeneo yao yanayochimbwa mchanga Tsh. 3,000/- wakati Serikali hupata faida ya Tshs 7,000 kwa tani moja.

(a) Je, Serikali inalifahamu hilo.

(b) Je, Serikali inamungaliaje mwananchi anaekodisha ardhi hiyo ambaye anapata mapato ya chini ukilinganisha na anayekodishwa.

(c) Je, Serikali inawaangaliaje wananchi wake wa kipato cha chini kutokana na gharama ya juu ya bei ya mchanga.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

17. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuja Micheweni wakati wa kampeni za uchaguzi Mkuu wa 2020 aliahidi kuipandisha hadhi hospitali ya cottage ya Micheweni na kuwa Hospitali ya Wilaya.

Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa ili kuendelea kuwaboreshea huduma wananchi wa Wilaya hii.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

21. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Asilimia 95 ya wakaazi wa Kojani ni watu wanaotegemea uvuvi wa samaki na mazao mengine ya baharini. Kwa kuwa kipindi cha bamvua masoko ya Wete, Chake na Konde hujazwa samaki kiasi ambacho bei huteremka kwa kiwango kikubwa na hatimaye wavuvi huuza samaki wao kwa bei ya chini na isiyokuwa na maslahi kwao.

Je, ni lini Serikali itaandaa utaratibu wa kuifanya bei ya samaki iwe imara (stable) katika kipindi cha mwaka mzima ili kuwaokoa kimaisha wavuvi wa Kojani pamoja na maeneo mengine ya nchi hii.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais**,** Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**17 Mei, 2021.** **KATIBU WA BARAZA**